**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAJI**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BARIA**

Telegrams “MAJI Tel No: 028-2700204S.L.P 64, Bariadi

Fax: 028-2700204, Baruapepe: mdbaruwasa@yahoo.com

# MKATABA MDOGO WA AJIRA ZA MAFUNDI

**KATI YA**

**MKURUGENZI MTENDAJI S.L.P 64, BARIADI, SIMIYU**

**NA**

**NHANDI NG’HOLONGO SANDU S.L.P 308, ITILIMA**

**KWA**

**KAZI YA UJENZI WA TANKI LA MAJI LENYE UJAZO WA 135$m^3$**

**MKATABA NA.BRD/UWASA/2021-2022/W/TNK/01**

**Novemba, 2021**

Scanned with CamScanner

**FOMU F2: MKATABA MDOGO WA AJIRA ZA MAFUNDI**

**KAZI YA KUJENGA TANKI LA MAJI LENYE UJAZO WA 135m³**

**MKATABA HUU** unafanyika leo tarehe 25.......... mwezi 11.................., 2021....

**BAINA YA**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BARIADI (BARUWASA)** S.L.P 64 (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri au BARUWASA") kwa upande mmoja;

**NA**

**NHANDI NG'HOLONGO SANDU S.L.P 308 Itilima** (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiriwa au Fundi") kwa upande mwingine.

**KWAMBA** kwa pamoja Mwajiri na Mwajiriwa watajulikana kama pande mbili za Mkataba.

**AMBAPO:**

a) Mwajiri ni Mamlaka ya maji wenye jukumu la kutekeleza ujenzi wa miradi ya maji mjini na kusimamia utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira mjini.

b) Mwajiriwa ni mtu binafsi anayefanya shughuli zake binafsi za ujenzi **Bariadi;**

c) Mwajiri anakusudia kumwajiri Mwajiriwa kwa kipindi cha muda mfupi wa siku 30;

d) Mwajiriwa anakubali matakwa ya Mwajiri na anakubali kwa hiari yake mwenyewe kuajiriwa kwa muda mfupi kama fundi wa kufyatua tofali

e) **MKATABA HUU UNASHUHUDIWA** kwa pande zote mbili kukubaliana kama ifuatavyo:

Scanned with CamScanner

## 1. MADHUMUNI YA MKATABA

Mkataba huu ni kwa ajili ya ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa 100m³ eneo la Nyamimbi Somanda. Mwajiriwa atapaswa kufanya kazi zifuatazo:

I. Kusafisha eneo la Kujenga tanki
II. Kufanya vipimo eneo la kujengea tanki *(foundation setting)*
III. Kuchimba msingi wa tanki pamoja na shimo la kuhifadhi maji
IV. Kuweka mawe *(hadcore filling)*
V. Kuweka nondo (BRC) na kumwaga zege kwenye sakafu ya tanki.
VI. Ujenzi wa ukuta wa tanki na chemba ya kutolea maji *(outlet chamber)*
VII. Kuweka mabomba ya kuingiza na kutoa maji kwenye tanki pamoja na ngazi.
VIII. Kuweka nondo na kumwaga zege juu ya tanki *(top slab)*
IX. Kupiga lipu nje na ndani pamoja
X. Kujenga uzio kuzunguka eneo la tanki
XI. kupaka rangi kwenye tanki

## 2. MUDA WA UTEKELEZAJI WA KAZI

Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 90, ambapo itaanza tarehe 25/11/2021 na itakamilika tarehe 25/2/2022

## MALIPO YA UTEKELEZAJI WA KAZI

**a)** Mwajiriwa atalipwa jumla ya kiasi cha Tshs **16,000,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu;

**b)** Malipo ya Mwajiriwa yatakuwa ni kwa fedha za kitanzania tu (*Tanzanian Shillings*);

**c)** Malipo hayo yatalipwa aidha kwa fedha taslimu au hundi ambayo italipwa benki;

**d)** Malipo ya Mwajiriwa yatalipwa kama ifuatavyo:

- Malipo ya awamu ya kwanza yatalipwa mara baada ya kujenga msingi na kumwaga zege Tsh **3,200,000/=** ambapo ni sawa na asilimia 20 ya kazi ya ujenzi wa tanki
- Malipo ya awamu ya pili yatalipwa mara baada ya kukamilisha kazi ya ujenzi wa ukuta wa tanki Tsh **8,000,000/=** ambapo ni sawana asilimia 50
- Malipo ya awamu ya tatu na ya mwisho yatalipwa mara baada ya kukamilisha kazi yote kwa mujibu wa mkataba kiasi cha Tsh **4,800,000/=** ambapo ni sawa na asilimia 30

**e)** Kabla ya malipo ya mwisho kufanyika, Mwajiriwa anapaswa kuwasilisha taarifa zote zinazohitajika na kufanya marejesho ya vifaa vyote vya kazi na fedha za mradi kama zitakuwepo.

## 3. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRI

Scanned with CamScanner

i) Mvua kuzidi kunyesha na kusababisha kushindwa kuingia site la kazi
j) Kucheleweshewa vitendea kazi (construction materials)
k) Kucheleweshwa kwa Malipo.

**KWA USHUHUDA HUU,** pande zote mbili zimeweka sahihi zao katika Mkataba huu siku na tarehe kama ilivyoonyeshwa hapa chini.

| **MWAJIRI (BABUWASA)** | **Shahidi:** |
|---|---|
| **Jina:** Mwidini Mosha | **Jina:** Chalinick W. Mbwambo |
| **Sahihi:** [signature] | **Sahihi:** [signature] |
| **Cheo:** MB | **Cheo:** Meneja Ufundi |
| **Tarehe:** 25/11/2021 | **Tarehe:** 25/11/2021 |

MKURUGENZI MTENDAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
BABATI

| **MWAJIRIWA (FUNDI)** | **Shahidi:** |
|---|---|
| **Jina:** NHANDI N. SANDU | **Jina:** PAUL MAMANEU |
| **Sahihi:** NG Nsandu | **Sahihi:** Mnyagu |
| **Cheo:** Fundi | **Cheo:** Fundi |
| **Tarehe:** 25-11-2021 | **Tarehe:** 25/11/2021 |

Scanned with CamScanner